

# MAFANIKIO DMI





MKUU wa Chuo cha Bahari (DMI), Dk. Tumaini Gurumo.

## Jinsi DMI ilivyobeba jukumu kuutangaza uchumi wa buluu

## Safari ya Chuo DMI kuanzia mwaka 1978

## Idadi ya wanaosoma kozi za ubaharia yapaa kwa kasi

MAFANIKIO DMI


MABAHARIA wakiwa katika picha ya pamoja wakati wa mahafali ya 19 ya Chuo cha Bahari, Dar es Salaam (DMI), mwaka jana.

# Jinsi DMI ilivyobeba jukumu kuutangaza uchumi wa buluu

**Na CHARLES MGANGA**

TANGU kuingia madarakani, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Awamu ya Nane inayoongozwa na Rais Dk. Hussein Mwinyi, imekuwa ikiweka mkazo mkubwa katika kukuza uchumi kupitia rasilimali za baharini.

Katika kuhakikisha inatoa kipaumbele hicho, Rais Dk. Mwinyi, aliamua kuunda Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi ambayo ni mahususi inayoshughulikia masuala ya rasilimali baharini.

Wakati akizungumza na mabalozi wateule, Ikulu ya Zanzibar, Oktoba 04, mwaka jana ambao walikwenda kujitambulisha kwake, Rais Dk. Hussein, alisema Zanzibar bado ina mahitaji makubwa ya uwekezaji katika Sekta ya Uchumi wa Buluu kupitia utalii, utalii na ufugaji wa vifaranga vya samaki.

Katika mazungumzo yake, aliwataka mabalozi kuzichangamkia fursa za uwekezaji katika nchi wanazoziwakilisha na kuwavutia wawekezaji kuja Zanzibar, lengo likiwa kuimarisha uchumi wa nchi unaochangia asilimia 30 ya pato la taifa.

Pamoja na mabalozi kupewa maelekezo hayo, Chuo cha Bahari Dar es Salaam, nacho kimebeba jukumu la kuendelea kuwa kitovu cha ubobezi wa kuendeleza dhana ya uchumi wa buluu.

Mkuu wa Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI), Dk. Tumain Gurumo, alitoa pongezi kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwa namna ilivyotoa kipaumbele katika uchumi wa buluu.

Dk. Tumaini, alieleza namna DMI ilivyoamua kubeba jukumu la kuutangaza uchumi wa buluu ambao una fursa nyingi zilizopo baharini ambazo baadhi ya nchi zingine hazina baraka hiyo.

«Pongezi kwa Serikali za Zanzibar kwa kuona fursa zilizopo baharini, lengo ni kujipatia faida za kiuchumi.Tuna bahari ambapo samaki waliopo wanauzwa nje ya nchi.

"Faida ni nyingi ambazo sisi DMI, tunapaswa kuzieleza kwa sababu ni jukumu letu kufanya hivyo,» alisema Dk. Tumaini.

Dk. Tumaini alisema kwa sababu, DMI ina wajibu wa kutoa elimu, ushauri, mafunzo na mambo mengine katika masuala yanayohusu bahari, wamekuwa wakifanya kongamano mwaka wa tatu kuhusu uchumi wa buluu.

Alieleza kuwa, mwaka huu, DMI itafanya Kongamano la Kimataifa, ambalo litawahusisha watalaamu kutoka maeneo mbalimbali barani Afrika na nchi zingine kwa lengo la kubadilishana uzoefu.

"Tutapata wasemaji waliobobea katika eneo la uchumi wa buluu, kama nchi ya Mauritius ilivyofanikiwa, tunataka kujifunza kutoka kwao.

"Wanapiga hesabu jinsi walivyofanikiwa kutoka chini hadi kati, kisha juu kutokana na matumizi mazuri ya maji,» alisema Dk. Tumaini.

Alifafanua zaidi kuwa, huo ni mkakati wa Afrika kuhakikisha bara linanufaika kutokana na rasilimali zake zilizopo katika bahari.

"Niliwahi kuandika kitabu kinachoelezea fursa za bahari, tena nilitumia lugha ya kiswahili Watanzania wengi waweze kusoma kilichomo. Miongoni mwa kazi zetu kama DMI ni kufanya utafiti na utoaji elimu kupitia maandiko kama hayo," alieleza Dk. Tumaini.

Machi 16, mwaka huu, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu Kongamano la Tatu la Kimataifa la Uchumi wa Buluu,Dk. Tumaini alitoa wito kwa Watanzania kushirikiana na DMI katika kufanikisha shughuli hivo itakayofanyika Julai 4 na 5, 2024,

> **"Niliwahi kuandika kitabu kinachoelezea fursa za bahari, tena nilitumia lugha ya kiswahili Watanzania wengi waweze kusoma kilichomo. Miongoni mwa kazi zetu kama DMI ni kufanya utafiti na utoaji elimu kupitia maandiko kama hayo**
>
> **Mkuu wa Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI), Dk. Tumaini Gurumo**



katika Ukumbi wa Kimataifa wa Julius Nyerere, Dar es Salaam.

Dk. Tumaini alisema kongamano hilo, linafanywa na DMI kwa kushirikiana na Chuo cha Regional Maritime University (RMU), kilichopo Ghana, lengo likiwa kukutanisha wadau wa uchumi wa buluu ili kujadiliana na kubadilishana uzoefu katika kukuza dhana ya uchumi wa buluu barani Afrika.

"Kongamano hili linaandaliwa na DMI kwa sababu ndiyo chuo pekee katika nchi kilichopewa dhamana ya kufundisha masuala yanayohusu bahari kwa upana wake.

**MKAKATI MWINGINE**

Katika mwendelezo wa mazungumzo yake na jarida hili hivi karibuni, Dk. Tumaini alisema DMI, inakusudia kupita katika maeneo kunakofanywa shughuli za uchumi wa buluu ili kubaini uhitaji unaopaswa kutolewa kwa wananchi.

Dk. Tumaini alisema hata wanapoandaa kozi mpya zinazopaswa kufundishwa, itawapa fursa kutambua uhitaji wa msingi wa watu hao.

"Tunashiriki kikamilifu katika kutangaza dhana ya uchumi wa buluu kwa sababu, hata tunapoitwa kutoa ushauri, tunafanya hivyo kupitia kamati za uanzishwaji sera za uchumi wa buluu na maeneo mengine ili kuisaidia serikali," alieleza Dk. Tumaini.

Hata hivyo, Dk. Tumaini, aliwataka Watanzania hasa vijana ambalo ndilo kundi kubwa kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi iliyofanyika mwaka 2022 na matokeo kuonyesha Watanzania wako 61,741,120 kwa Tanzania Bara na Visiwani kuchangamkia fursa za Ubaharia.

Alitoa wito kwa wazazi na walezi, kuondoa dhana kuwa ubaharia ni uhuni, na kwamba wanapaswa kutambua ni fani kama zilivyo nyingine na kuna fursa nyingi hivi sasa.

Alizitaja fursa zilizopo sasa kuwa ni ujenzi wa meli kwani kwa sasa DMI inatoa kozi ya Usanifu wa Meli, mafuta na gesi vinachimbwa Tanzania, hivyo vijana wasipochangamka na kuingia katika kada za ubaharia, itatoa mwanya watu kutoka nchi zingine kufanya kazi zinazoweza kufanywa na wazawa.

"Miongoni mwa wanaosoma hapa chuoni niraia wanaotoka nje ya Tanzania, sasa ni vyema nafasi katika miradi mbalimbali, zikachukuliwa na Watanzania, siyo raia wengine wa kigeni.

MAFANIKIO DMI

# Safari ya Chuo DMI kuanzia mwaka 1978




**Naibu Waziri wa Uchukuzi, David Kihenzile, akizungumza na wahitimu wa Mahafali ya 19 ya Chuo cha Bahari Dar es Salaam, mwaka jana.**

**Na MWANDISHI WETU**

CHUO cha Bahari Dar es Salaam (DMI), kilianzishwa mwaka 1978 baada ya kuvunjika Umoja wa Nchi za Afrika Mashariki (EAC).

Akizungumzia historia kwa ujumla ya DMI, Mkuu wa Chuo hicho, Dk. Tumaini Gurumo, alisema wakati wa Umoja wa Jumuiya ya Nchi za Afrika Mashariki, shughuli zilikuwa zikifanywa kwa pamoja, ikiwemo usafirishaji.

Alisema baada ya kuvunjika umoja huo, Tanzania ilibahatika kupewa meli, lakini ikagundulika hakukuwa na Watanzania ambao wangeweza kuziendesha.

"Baada ya kugawiwa meli, ilibainika kwamba, hakukuwa na Watanzania ambao wanaoweza kupewa kuziendesha meli hizo, kwani tulikuwa hatuna manahodha,» alisema Dk. Tumaini.

Dk. Tumaini, alisema waliokuwa viongozi wakati huo, waliona umuhimu wa kuwa na Watanzania wenye sifa, ingawa awali, walitumika wataalamu kutoka nje ya nchi.

Alisema baadae, ukaanzishwa utaratibu wa Tanzania kuwa na chuo cha bahari, lengo likiwa kuwafundisha Watanzania, kwa sababu kusoma taaluma hiyo nje ya nchi ni gharama kubwa.

**"Baada ya kubaki na meli, ilibainika kwamba, hakuna Watanzania wanaoweza kupewa kuendesha meli hizo, kwani hatukuwa na manahodha wala wahandisi," alisema Dk. Tumaini.**

Alieleza kuwa, kutokana na umuhimu huo, chuo hicho cha bahari, kilianza kama kitengo, kilichokuwa chini ya Wizara ya Uchukuzi, kilianza kufundisha mabaharia kwa ngazi za chini.

**FANI YA UBAHARIA**

Kwa mujibu wa Dk. Tumaini, ubaharia ni fani kama zilivyo nyingine, ina ngazi zake kama taaluma nyingine ambapo mhusika huanzia chini na kupanda hatua kwa hatua.

Alifafanua zaidi kuwa, mabaharia hao, wanatofautiana kulingana na elimu walizopata na ukubwa wa chombo ambacho atakachofanyia kazi.

Alieleza kuwa, chuo kilipoanzishwa, walikuwa wakitoa mafunzo kwa mabaharia wa ngazi saidizi hadi ngazi ya afisa daraja la tatu. Kwa sasa Chuo kinatoa mafunzo hadi ngazi ya daraja la kwanza kwa manahodha (Master Mariners) na wahandisi wa meli (Marine Chief Engineers).

**MWAKA 2003**

Kwa mujibu wa Dk. Tumaini, mwaka 2003, ubora wa mafunzo yanayotolewa na Chuo ulifanikisha Nchi ya Tanzania kuingizwa katika orodha ya 'White List' hivyo, kuwezesha mabaharia wanaohitimu hapa nchini kutambulika kimataifa na kupata kazi nchi yoyote duniani.

Alisema kuwa, hatua ya uingiaji katika 'white list' ni mchakato kwani, zipo baadhi ya nchi, hazijafikia hivyo.

"Kwetu ni mafanikio makubwa kwa sababu, kuna nchi jirani hadi sasa hazijafanikiwa kuingia katika 'white list,' lakini Tanzania kama nchi tumefanikiwa kuwemo tangu mwaka 2003.

Aidha, Dk.Tumaini, alisema kuwa, kimsingi elimu ya ubaharia, unahitaji wanafunzi kufanya vitendo baada ya nadharia ya darasani, hivyo vifaa vinahitaji zaidi.

Hata hivyo, kabla ya kuingia katika 'White List', kulifanyika juhudi kubwa ya kuwa na vifaa vya kisasa vya kufundishia kwa sababu elimu ya ubaharia imejikita katika vitendo zaidi kuliko nadharia.

"Tunapofundisha darasani, kuna wakati unafika kwenda kufanya vitendo, sasa hatua ya vitendo inahitaji zaidi kuwa na mitambo ya 'Simulators,' alisema Dk. Tumaini.

**MITAMBO NA VIFAA VYA KUFUNDISHIA**

Akifafanua zaidi kuhusu mitambo hiyo, Dk. Tumaini alisema ipo ambayo ina kila kitu kinachoweza kupatikana katika meli.

"Hata ule upande wa chumba cha nahodha ambacho anakitumia, nako kuna kila kitu," alisisitiza Dk. Tumaini.

Alisema kuwa na mitambo hiyo pamoja na karakana ya uhandisi ni miongoni mwa vigezo na sifa zilizofanya chuo kuendelea kuboresha utoaji wa elimu na mafunzo kwa vitendo katika tasnia ya bahari.



**MABAHARIA Wakufunzi wa DMI wakiangalia mtambo wa mafunzo kwa vitendo kwa wahandisi wa meli (Engine Room Simulator)**

MAFANIKIO DMI

# Idadi ya wanaosoma kozi za ubaharia yapaa kwa kasi

**>>Walianza** na wanafunzi 12 chuo kilipoanzishwa, hivi sasa wafikia 5,177

**Na CHARLES MGANGA**

CHUO cha Bahari Dar es Salaam (DMI), kilianza kutoa mafunzo ya ubaharia na uhandisi kikiwa na wanafunzi 12.

Kadri miaka iliyoongezeka, idadi na mwitikio wa wanafunzi kutaka kusomea taaluma hizo, uliendelea kuongezeka.

Mwaka jana, katika Maonyesho ya Biashara ya Kimataifa, maarufu kama Sabasaba, wananchi wengi hasa kada ya vijana, walijitokeza katika banda la DMI, wakitaka kufahamu mambo mbalimbali na utaratibu wa kujiunga.

Julai 12, mwaka jana, akiwa katika banda hilo, Viwanja vya Mwalimu Julius Nyerere jijini Dar es Salaam, Mkuu wa Udahili wa Chuo hicho, Bernard Mgendwa, alisema kwamba, kumekuwa na mwitikio mkubwa kwa vijana, kujitokeza kutaka kujiunga na chuo hicho katika fani mbalimbali ikiwemo ya ubaharia.

Mgendwa alisema kuwa, chuo hicho, kimeshiriki maonesho hayo kueleza shughuli za kitaaluma na fursa zinazotokana na Uchumi wa Buluu kupitia Bahari, Mito na Maziwa.

Alieleza kuwa, DMI imekuwa ikitoa kozi na programu mbalimbali za bahari kwa watu binafsi na nchi mbalimbali za jirani, zikiwemo, Kenya, Uganda, Comoro, Rwanda, Burundi, Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na Namibia.

Aidha, DMI inatambulika kwa programu zake za mafunzo ya ubora wa hali ya juu katika taaluma ya bahari kwa kufuata viwango vya kimataifa.

Akizungumza na jarida hili jijini Dar es Salaam hivi karibuni, Mkuu wa Chuo hicho, Dk. Tumaini Gurumo, alisema kwamba, kumekuwa na mwamko mkubwa wa Watanzania kutaka kusoma taaluma ya bahari, ikilinganishwa na ilivyokuwa wakati DMI inaanzishwa mwaka 1978.

Dk. Tumaini, alisema kwa mwaka 2024, wanafunzi wamefikia idadi ya 5,177 wa kozi ndefu na 6,000 wa kozi fupi huku idadi ikiendelea kuongezeka kila mwaka.



MKUU wa Chuo cha Bahari (DMI), Dk. Tumaini Gurumo.

Akieleza kasi ya ongezeko hilo, Dk. Tumaini alisema mwaka jana mwaka wa masomo wa 2022/2023 , wanafunzi walikuwa 3,505 huku mwaka 2021/2022, walikuwa 2,299, na mwaka 2020/2021 walikua 1,590 hali inayoonyesha chuo kupiga hatua kubwa.

**MWAMKO ZAIDI ZANZIBAR**

Dk. Tumaini, alisema kuwa, licha ya kuwepo kasi hiyo ya ongezeko la idadi ya wanafunzi, vijana kutoka visiwani Zanzibar, ndiyo wameonekana kuwa na mwamko mkubwa ikilinganishwa na wanaotoka Tanzania Bara.

"Wanaotoka Zanzibar ndiyo wanajiunga wengi chuoni ukilinganisha na huku Bara.

"Sababu ya wao kuwa na mwamko mkubwa, inatokana na shughuli zao nyingi kutegemea bahari.

"Unajua Zanzibar ni kisiwa, hivyo wakazi wa huko, kazi zao nyingi zinatokana na uvuvi.

"Hivyo, wao ndiyo wamekuwa na shauku zaidi ya kutaka kusoma masuala ya bahari ukilinganisha na vijana wa Tanzania bara," alifafanua Dk. Tumaini.

**HAMASA TANZANIA BARA**

Alisema kuwa, zimekuwa zikifanyika jitihada za makusudi kuhakikisha Watanzania au vijana kutoka Tanzania Bara, wanajiunga na Chuo cha Bahari.

Dk.Tumaini alisema inawezekana hapo awali vijana hawakuwa wakiziona fursa katika bahari, lakini mwitikio unaendelea kuimarika mwaka hadi mwaka.

**MAJUKUMU MENGINE YA DMI**

Kwa mujibuwa Dk. Tumaini, Sheria Namba 22 ya mwaka 1991 iliyoanzishwa kwa Sheria ya Bunge, ilitoa majukumu kwa DMI kama Taasisi ya Elimu ya Juu na kupewa kazi muhimu, mojawapo ikiwa ni kutoa elimu na mafunzo.

Pamoja na kuendelea na jukumu la kufundisha, DMI pia inahusika 'kupika' rasilimali watu katika maeneo yote ya shughuli za maji.



Wanafunzi wa fani ya Uhandisi wa meli wakiwa kwenye karakana ya mafunzo kwa vitendo

MAFANIKIO DMI


WANAFUNZI wakijisomea katika Chumba cha Maktaba chuoni hapo.

# Kasi wanaosoma taaluma ya ubaharia DMI yapaa

**UHUSIANO WA TASAC NA DMI**

Dk. Tumaini, alisema kwa sababu Tanzania ilisaini mkataba wa kimataifa unaoongoza au kusimamia mafunzo ya mabaharia, ilipaswa kuwa na mamlaka inayojitegemea .

Aliendelea kueleza kuwa, ilianzishwa Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Majini (TASAC), ambayo pamoja na mambo mengine, ndiyo msimamizi wa ndani.

"TASAC inahusika kuangalia mitaala ya kozi mbalimbali zinazofundishwa na chuo chetu.

"Lazima ipitie mitaala yetu kisha kuridhia kutumika baada ya kufuata vigezo vyote vya kimataifa vinavyohitajika," alisema mkuu huyo wa chuo.

Aidha, alisema kwamba, hata mitihani inapoandaliwa, kabla wanafunzi hawajaanza kuifanya, TASAC huwa na jukumu la kuikagua kwanza.

Alisema lengo la TASAC kufanya hivyo, ni kuhakikisha ubora wenye kiwango cha kimataifa, unazingatiwa.

"Huwa tunakaguliwa na TASAC kama tuna rasilimali watu wa kutosha, hiyo ni kutokana na sheria ya kimataifa inavyoelekeza. Pia, huangaliwa kama tuna vifaa vya kutosha.

Pia, alieleza hata 'International Maritime Organization' (IMO), ambao ndiyo wenye sheria za ubaharia, huwa na kawaida ya kuja nchini kila baada ya miaka mitano kufanya ukaguzi.

Dk. Tumaini alieleza kwamba, ujio wa IMO nchini, hujikita zaidi kutoa ushauri na maoni mbalimbali

**USHIRIKIANO NA TAASISI NA VYUO VYA NJE**

Dk. Tumaini, alisema DMI, imekuwa na uhusiano na Taasisi au Vyuo mbalimbali nje ya nchi, hatua ambayo chuo imekuwa ikinufaika.

Baadhi ya nchi alizozitaja kuwa na ushirikino ni pamoja na China, Norway, Italia, Korea Kusini na Ghana.

Alifafanua miongoni mwa manufaa wanayopata kupitia ushirikiano huo, mojawapo ni wanafunzi kupata nafasi katika meli za kufanyia mafunzo kwa vitendo.

"Unajua sisi hatuna meli za kufanyia mafunzo, sasa kutokana na uhusiano na ushirikiano uliopo, wanafunzi wetu wanapata nafasi katika meli za wenzetu ambao wanazo.


Jengo la Chuo Cha Bahari (DMI)

**DMI YAIPONGEZA SERIKALI**

Dk. Tumaini, aliishukuru Serikali kwa kutambua uhitaji wa rasilimali watu ambao wamekuwa wakiongezwa kila inapohitajika.

Alisema wapo walimu wanaofundisha kwa muda maalumu, lakini licha ya uchache wao, wana weledi mkubwa unaojitosheleza.

Pia, DMI imekuwa ikitumika kutoa ushauri kwa serikali na kampuni binafsi kuhusu masuala ya maji kwani hata meli zinazojengwa na kukaguliwa, baadhi ya wataalamu hutoka chuoni hapo.

**MKUU WA CHUO MZAWA**

Dk. Tumaini, alisema mwaka 1990, DMI ilipata mkuu wa chuo wa kwanza mzawa, baada ya kuongozwa na raia wa Norway tangu kuanzishwa kwake kwani kabla ya kipindi hicho, Watanzania hawakuwa na uwezo huo.

Alieleza kuwa, katika kuzingatia masuala ya jinsia, mwaka jana, yeye aliteuliwa kuwa mkuu wa chuo wa kwanza, mwanamke.

**KUHUSU DK. TUMAINI:**

Dk. Tumaini, ambaye ni mkuu wa chuo hicho wa kwanza mwanamke, ni mhadhiri mwandamizi na amekuwa akifundisha chuoni hapo, tangu mwaka 2005.

Awali, alikaimu nafasi ya mkuu wa chuo kwa miaka miwili mfululizo kabla ya kuteuliwa rasmi kuongoza DMI.

Kwa mujibu wa taarifa za kimtandao, Dk. Tumaini ana uzoefu mkubwa katika masuala ya bahari.

Pia, anafundisha kozi mbalimbali zikiwemo za sheria za bahari, masuala ya bima na ubebaji mizigo baharini.

Amewasimamia wanafunzi wengi huku naye akishiriki katika kuandaa kanuni, sera na mengine yanayohusu bahari.

Dk. Tumaini ndiye mtunzi wa kitabu alichokipa jina; "UCHUMI WA BLUU: Fursa na Chachu ya Maendeleo."

**MIKAKATI MINGINE**

Dk. Tumaini, alisema kwamba, licha ya kupata eneo la kujenga tawi la chuo Pemba, kuna mkakati wa kuongeza wigo katika mkoa ya Lindi ambako elimu inahitajika kutokana na uwepo wa gesi na mafuta ambavyo vinachimbwa baharini.

"Mipango ya miaka ijayo ni kuangalia eneo la Lindi ambako kumepatikana kiwanja, pia mikoa ya Mwanza , Simiyu na Pwani " alisema Dk. Tumaini.